# JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

## WIZARA YA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA

# MWONGOZO WA KITAIFA WA KUONGEZA FURSA ZA UFADHILI WA MASOMO NDANI NA NJE YA NCHI

**Oktoba, 2025**

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**WIZARA YA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA**

# MWONGOZO WA KITAIFA WA KUONGEZA FURSA ZA UFADHILI WA MASOMO NDANI NA NJE YA NCHI

**Oktoba, 2025**

# YALIYOMO


**ORODHA YA MAJEDWALI** ........................................ **iv**

**DIBAJI** ........................................ **v**

**VIFUPISHO** ........................................ **vi**

**SURA YA KWANZA** ........................................ **1**

**1. UTANGULIZI** ........................................ **1**

1.1 Usuli ........................................ 1

1.2 Hali ya Sasa ........................................ 1

1.3 Chimbuko ........................................ 2

1.4 Umuhimu wa Mwongozo ........................................ 3

1.5 Malengo ya Mwongozo ........................................ 3

1.5.1 Lengo Kuu ........................................ 3

1.5.2 Malengo Mahususi ........................................ 3

1.6 Mikakati ya Kutimiza Malengo ........................................ 4

1.7 Muundo wa Mwongozo ........................................ 4

1.8 Utaratibu wa Kuandaa Mwongozo ........................................ 5

1.8.1 Mapitio ya Nyaraka ........................................ 5

1.8.2 Kukusanya Maoni ya Wadau ........................................ 5

1.9 Walengwa ........................................ 5

**SURA YA PILI** ........................................ **6**

**2. UTARATIBU WA KUONGEZA FURSA ZA UFADHILI WA MASOMO NDANI NA NJE YA NCHI** ........................................ **6**

2.1 Fursa za Ufadhili wa Masomo Ndani na Nje ya Nchi ........................................ 6

2.1.1 Madhumuni ya Ufadhili wa Masomo Ndani na Nje ya Nchi ........................................ 6

2.1.2 Aina za Fursa za Ufadhili wa Masomo Ndani na Nje ya Nchi ........................................ 7

2.1.3 Namna ya Kupata Fursa za Ufadhili wa Masomo Ndani na Nje ya Nchi ........................................ 7

2.2 Mahitaji ya Fursa za Ufadhili wa Masomo Ndani na Nje ya Nchi ........................................ 7

2.2.1 Kubainisha Maeneo na Fani za Kimkakati ya Nchi kwa Ajili ya Kutafuta Ufadhili wa Masomo Ndani na Nje ya Nchi ........................................ 7

2.2.2 Kubainisha Nchi Hisani Zenye Umahiri katika Fani za Kimkakati Zinazohitajika Nchini kwa Ajili ya Ufadhili wa Masomo ........................................ 8

2.2.3 Kubainisha Maeneo ya Ushirikiano Ambayo Taasisi za Elimu, Dini na Mashirika Yasiyo ya Kiserikali Yanapata au Kutoa Ufadhili wa Masomo Ndani na Nje ya Nchi ........................................ 8

2.2.4 Kubainisha Fani Ambazo kwa Umuhimu na Unyeti Wake, Serikali Itawafadhili Watanzania Kusoma Ndani na Nje ya Nchi ........................................ 8

2.3 Kubainisha Fursa za Ufadhili wa Masomo Ndani na Nje ya Nchi ..... 9
2.3.1 Ushirikiano ..... 9
**2.3.2 Balozi za Ndani na Nje ya Nchi ..... 9**
**2.3.3 Taasisi za Uwakala wa Elimu ..... 9**
**2.3.4 Watanzania Waishio Nje ya Nchi (Diaspora) ..... 9**
**2.3.5 Makampuni, Wafanyabiashara, Mashirika ya Dini na Watu Binafsi ..... 10**
**2.3.6 Viongozi wa Serikali ..... 10**
2.4 Kutangaza Fursa za Ufadhili wa Masomo Ndani na Nje ya Nchi ..... 10
2.4.1 Kuboresha Njia za Kutangaza Fursa za Ufadhili ..... 10
2.4.2 Kushiriki na Kuandaa Makongamano na Maonesho ..... 11
2.4.3 Ukurasa Mahususi wa Fursa za Ufadhili wa Masomo Ndani na Nje ya Nchi 11
2.4.4 Jumuiya na Mashirika ya Kijamii ..... 11
2.5 Usimamizi wa Fursa za Ufadhili wa Masomo Ndani na Nje ya Nchi ..... 11
2.5.1 Dawati Maalumu kwa Ajili ya Usimamizi wa Fursa za Ufadhili wa Masomo Ndani na Nje ya Nchi ..... 11
2.5.2 Uhakiki na Uidhinishaji wa Fursa ..... 12
2.5.3 Kupokea Fursa na Kuongeza Uelewa ..... 12
2.5.4 Taasisi za Wakala wa Elimu ..... 12
2.5.5 Mfumo wa Taarifa na Mrejesho ..... 12
2.5.6 Kuunganisha Mifumo ya Kidijitali ..... 12
2.6 Kujenga Uwezo ..... 13
2.6.1 Waombaji wa Ufadhili wa Masomo Ndani na Nje ya Nchi ..... 13
2.6.2 Waratibu wa Fursa za Ufadhili wa Masomo Ndani na Nje ya Nchi ..... 13
**SURA YA TATU ..... 14**
**3. MAJUKUMU ..... 14**
3.1 Majukumu ya Serikali ..... 14
3.2 Majukumu ya Balozi ..... 14
3.3 Majukumu ya Taasisi za Elimu ..... 15
3.4 Majukumu ya Taasisi za Uwakala wa Elimu ..... 15
**SURA YA NNE ..... 16**
**4. UFUATILIAJI NA TATHMINI ..... 16**
**Jedwali Na. 1: JEDWALI LA UTEKELEZAJI, UFUATILIAJI NA TATHMINI YA MWONGOZO WA KUONGEZA FURSA ZA UFADHILI WA MASOMO NDANI NA NJE YA NCHI ..... 17**
**Marejeleo ..... 26**

# ORODHA YA MAJEDWALI

Jedwali Na. 1: JEDWALI LA UTEKELEZAJI, UFUATILIAJI NA TATHMINI YA MWONGOZO WA KUONGEZA FURSA ZA UFADHILI WA MASOMO NDANI NA NJE YA NCHI ............................................................. 17

# DIBAJI

Elimu ni nguzo muhimu katika maendeleo ya taifa lolote. Inatoa misingi ya ufahamu, ujuzi, na umahiri katika kutekeleza majukumu ya kijamii, kiuchumi, na kisiasa. Kwa kuzingatia umuhimu huu, Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania imekuwa ikitekeleza mikakati mbalimbali ya kukuza na kuendeleza sekta ya elimu ili kuhakikisha inakidhi mahitaji ya soko la ajira, maendeleo ya kijamii, na ushindani wa kimataifa.

Mwongozo wa Kitaifa wa Kuongeza Fursa za Ufadhili wa Masomo Ndani na Nje ya Nchi umeandaliwa kama sehemu ya juhudi za Serikali kuimarisha mifumo ya elimu na kuleta mabadiliko chanya katika ufadhili wa masomo katika nyanja zote ikiwemo sayansi, teknolojia na ubunifu. Mwongozo huu unalenga kutatua changamoto zilizopo katika upatikanaji wa rasilimali za elimu kwa wanafunzi, hasa katika fani za sayansi, teknolojia, uhandisi, na ubunifu, ambazo ni muhimu kwa maendeleo endelevu ya nchi na bara zima la Afrika.

Mwongozo wa kuongeza fursa za ufadhili wa masomo unaongeza wigo wa watanzania kupata elimu bora, ya viwango vya kimataifa, na kuwa tayari kuchangia katika maendeleo ya jamii, sekta binafsi, na taifa kwa ujumla. Mwongozo huu unatoa mifumo na taratibu za kuongeza fursa za ufadhili kwa ushirikiano kati ya serikali, sekta binafsi, na mashirika ya kimataifa katika kuongeza ufadhili wa Masomo ndani na nje ya nchi.

Mwongozo una Sura nne. Sura ya Kwanza inahusu utangulizi. Sura ya Pili inahusu utaratibu wa kuongeza fursa za ufadhili wa masomo ndani na nje ya nchi. Sura ya Tatu inahusu majukumu ya wadau. Sura ya Nne ni ufuatiliaji na tathmini katika utekelezaji wa mwongozo wa kuongeza fursa za ufadhili wa masomo ndani na nje ya nchi.

Prof. Carolyne I. Nombo

**KATIBU MKUU**

**WIZARA YA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA**

# VIFUPISHO

| | |
|---|---|
| NACTVET | National Council for Technical and Vocational Education and Training |
| NECTA | National Examination Council of Tanzania |
| STISA | Science, Technology and Innovation Strategy for Africa |
| TAHILISO | Tanzania Higher Learning Institutions Students Organization |
| TCU | Tanzania Commission for Universities |
| WyEST | Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia |
| CCM | Chama cha Mapinduzi |
| UNESCO | United Nations Education, Science and Cultural Organization |
| TEHAMA | Teknolojia ya Habari na Mawasiliano |
| NGOs | Non-Governmental Organizations |
| COSTECH | Commission for Science and Technology |
| MFAEC | Ministry of Forein Affairs and East African Cooperation. |

# SURA YA KWANZA

## 1. UTANGULIZI

### 1.1 Usuli

Umoja wa Afrika kupitia Agenda yake ya Maendeleo ya 2063 (The Africa We Want), imeweka shabaha ya kuwa na watu walioelimika na wenye ujuzi na umahiri katika nyanja zote ikiwemo sayansi, teknolojia na ubunifu. Ili kufikia shabaha hiyo, Umoja wa Afrika unatekeleza Mpango Mkakati wa kuendeleza Sayansi, Teknolojia na Ubunifu (STISA - 2024). Mkakati huu umedhamiria kufanya mabadiliko ya kijamii na uchumi kwa kuwekeza katika elimu ili kuinua viwango vya umahiri, ubunifu na maboresho kwenye uzalishaji viwandani na ujasiriamali. Ili kutimiza dhamira hii, STISA 2024 imeweka lengo la kuvifanya vyuo vikuu vya Afrika kuwa taasisi za umahiri kwa kuwekeza katika ujenzi wa miundombinu na kuzalisha wahitimu wenye umahiri na ujuzi wa viwango vya kikanda na kimataifa.

Kwa kutambua umuhimu wa utekelezaji wa mkakati huu kikanda na kimataifa, Serikali imeweka mwongozo wa kitaifa wa kuongeza fursa kupitia Sera ya Elimu na Mafunzo ya 2014 Toleo la 2023. Sera hii ni mwongozo unaolenga kuinua ubora wa elimu na mafunzo kwa kuweka mifumo na taratibu zitakazowezesha kupata idadi ya watanzania walioelimika, wenye stadi na wanaopenda kujiendeleza kielimu ili waweze kuchangia katika maendeleo endelevu ya kitaifa.

Sambamba na utekelezaji wa sera hii na mipango ya kitaifa, serikali inatekeleza ilani ya Chama cha Mapinduzi ya mwaka 2025 ambayo katika elimu, imeweka lengo la kuzalisha wataalamu mahiri na wenye uwezo katika uga wa sayansi, teknolojia, ufundi na nyuga nyingine ambazo zitaweza kuwasaidia wataalamu hao kuajriwa mahali popote Duniani. Ilani hiyo ya Chama cha Mapinduzi husussani, inaielekeza Serikali kuwawezesha wahitimu katika ngazi zote kujiajiri au kuajiriwa kitaifa na kimataifa.

Ili kufikia malengo yaliyoainishwa hapo juu, Serikali imeongeza fursa za mafunzo katika nyanja mbalimbali za  elimu ili kuruhusu wahitimu kwenda kusoma ndani na nje ya nchi. Sambamba na ongezeko la udahili, Serikali imeongeza ufadhili wa wanafunzi wa elimu kupitia mikopo ya elimu. Hata hivyo, idadi hiyo ni ndogo ikilinganishwa na uhitaji na idadi ya wanafunzi wanaohitimu kutoka elimu ya sekondari na vyuo vya ufundi.

### 1.2 Hali ya Sasa

Kwa kipindi cha miaka kumi iliyopita (2013-2022) takwimu zinaonesha idadi ya wanafunzi wanaohitimu elimu ya msingi imekuwa ikiongezeka mwaka hadi mwaka. Takwimu hizo zinaonesha kuwa Mwaka 2013 wanafunzi waliohitimu elimu ya msingi walikuwa ni 427,606 ambapo mwaka 2022 idadi ya wahitimu iliongezeka hadi kufikia

1,073,402. Mwaka huo huo 2022 kati ya wanafunzi 1,073,402 waliohitimu darasa la saba, wanafunzi 1,019,879 tu ndio waliopata nafasi za kujiunga na elimu ya sekondari, hii ni sawa na asimilia 95.0 ya wanafunzi wote waliohitimu elimu ya msingi kwa kipindi tajwa.

Idadi kubwa ya wanafunzi wanaohitimu elimu ya sekondari na kufaulu imepelekea kuwepo kwa ongezeko la wanafunzi wanaoomba kujiunga na elimu ya juu au elimu ya kati. Kwa mfano, katika mwaka 2012/2013 jumla ya wanafunzi 83,325 walipata nafasi za udahili katika taasisi mbalimbali za elimu ya juu na Vyuo Vikuu nchini, mwaka 2021/2022 idadi ya wanafunzi waliopata udahili katika Vyuo Vikuu na taasisi za elimu ya juu iliongezeka kufikia 183,098 ikiwa ni ongezeko la takribani wanafunzi 99,773. Katika hatua za kukabiliana na ongezeko la idadi ya wanafunzi wanaohitimu na kufaulu mitihani yao katika ngazi mbalimbali za elimu, Wizara imekuwa ikiendelea kuongeza miundombinu katika taasisi za elimu nchini kupitia fedha za maendeleo na miradi mbalimbali ya kuboresha elimu.

Pamoja na uboreshaji huo wa miundombinu, Wizara imeona umuhimu wa kutafuta nafasi zaidi za ufadhili wa masomo katika taasisi mbalimbali za elimu ndani na nje ya nchi ili kupata wataalamu katika fani mbalimbali zilizopewa kipaumbele na Serikali.

Katika kuthibitisha jitihada za kutafuta nafasi na ufadhili kutoka kwenye mashirika na nchi hisani kila mwaka, wizara imekuwa ikipokea na kuratibu zaidi ya nafasi 150 za ufadhili wa masomo kutoka katika baadhi ya nchi za bara la Ulaya, Asia na Afrika. Kwa kipindi cha miaka minne iliyopita yaani kuanzia 2019/2020-2022/2023, Watanzania 357 walinufaika na fursa za ufadhili wa masomo kutoka katika nchi mbalimbali.

Watanzania walionufaika na ufadhili huo kutoka nchi ya Uingereza ni 27, Hungary 78, Urusi 20, China 137, Algeria 18, Misri 47, Morocco 26 na Mauritius 4. Kuanzia mwaka wa masomo 2022/2023 Wizara imepokea nafasi mpya 88 kutoka Jamhuri ya Watu wa China, na nafasi 30 kutoka Hungary. Hata hivyo, idadi ya nafasi zinazopatikana ni chache sana ukilinganisha na mahitaji ya nchi na wingi wa nafasi hizo duniani.

## 1.3 Chimbuko

Dira ya Taifa ya Maendeleo ya 2050 imebainisha wazi kwamba Tanzania inapaswa kujizatiti katika kujenga ubunifu, ustadi, na elimu bora ili kukabiliana na changamoto za kimaendeleo na kushindana kikamilifu kikanda na kimataifa. Kwa kuzingatia dhamira hii, Sera ya Elimu na Mafunzo ya mwaka 2014 (Toleo la 2023) inalenga kuiwezesha nchi kuwa na elimu na mafunzo yenye viwango vya ubora vinavyotambulika kitaifa, kikanda, na kimataifa.

Pamoja na hatua mbalimbali za maendeleo zilizobainishwa, maboresho yanayoendelea kufanyika katika mitaala ya elimu na ujenzi wa miundombinu, bado idadi ya wanafunzi wanaodahiliwa katika elimu ya juu ni ndogo ikilinganishwa na mahitaji. Kwa mfano,

katika mwaka wa masomo wa 2023/2024 jumla wa wanafunzi 144,755 waliomba kujiunga na taasisi za elimu ya juu ambapo 133,617 walidahiliwa na waliopata mikopo toka Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu nchini ni 77,167 sawa na asilimia 58 tu.

Ili kuongeza fursa za udahili na ufadhili, kuna haja ya kuwezesha watanzania wengi zaidi kupata na kutumia fursa za ufadhili zinazotolewa na wafadhili mbalimbali ikiwemo mashirika ya kikanda na kimataifa, taasisi binafsi na taasisi za kidini. Kwa sasa fursa zinazopatikana ni chache ukilinganisha na udahili unaofanyika. Kwa mfano, kuanzia mwaka 2019/2020 hadi 2022/2023 jumla ya watanzania takribani 357 walinufaika na fursa za ufadhili wa masomo kutoka katika nchi mbalimbali kupitia Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia. Aidha, ni muhimu serikali kuwa na mfumo wa kuwatambua wanufaika wa fursa hizo za ufadhili, fani wanazosomea na nchi wanazokwenda ili nchi iweze kuwa na taarifa sahihi za rasilimali watu wake na ujuzi uliopo. Vilevile, taarifa hizo ni muhimu sana kwa usalama wa nchi yetu.

Hivyo,ili kuratibu upatikanaji wa fursa na utambuzi wa wanufaika wa fursa hizo, kuna umuhimu wa kuwa na mwongozo utakaojumuisha mbinu na hatua za kuchukuliwa ili kuongeza uelewa na upatikanaji wa fursa hizo.

## 1.4 Umuhimu wa Mwongozo

Mwongozo huu utaiwezesha nchi kutumia na kunufaika na fursa zinazotolewa kwa lengo la kuwasomesha watanzania wengi katika maeneo ya fani za kimkakati kulingana na mahitaji ya nchi. Aidha, Mwongozo huu utawawezesha watanzania wengi kusoma katika nchi zenye ubobevu katika maeneo mahususi ya taaluma kama vile akili mnemba, udaktari bingwa, uhandisi wa ndege, meli, treni, magari na maeneo mengine muhimu kwa maendeleo ya nchi yetu. Vilevile, mwongozo huu utawezesha upatikanaji wa maarifa, ujuzi na uzoefu unaohitajika pamoja na kuhaulisha maarifa ya sayansi, teknolojia na ubunifu kutoka nchi watakazosoma na kuzileta nchini.

## 1.5 Malengo ya Mwongozo

Mwongozo huu una lengo kuu moja na malengo mahususi sita.

### 1.5.1 Lengo Kuu

Lengo kuu la mwongozo huu ni kuongeza upatikanaji wa fursa za ufadhili wa masomo ndani na nje ya nchi.

### 1.5.2 Malengo Mahususi

i. Kuweka utaratibu wa uratibu na usimamizi wa fursa za masomo ndani na nje ya nchi;

ii. Kuweka utaratibu wa ubainishaji wa mahitaji ya fursa za ufadhili katika maeneo ya kimkakati ya kitaifa kiuchumi na kimaendeleo;

iii. Kuweka utaratibu wa upatikanaji na usambazaji wa taarifa za fursa za masomo zinazopatikana ndani na nje ya nchi katika taasisi mbalimbali;

iv. Kujenga uwezo kwa waratibu wa fursa za masomo ndani na nje ya nchi;

v. Kujenga uwezo na kutoa elimu ya mbinu bora za kufanya maombi ya ufadhili wa masomo ndani na nje ya nchi; na

vi. Kuweka mfumo wa kuwatambua na kuwafuatilia watanzania wanaopata fursa za masomo ndani na nje ya nchi;

## 1.6 Mikakati ya Kutimiza Malengo

Ili kuweza kufikia malengo yaliyowekwa, ni vyema Serikali, kwa kushirikiana na wadau, ikahakikisha kunakuwa na upatikanaji wa taarifa, uelewa, na uratibu mzuri wa mifumo wezeshi kwa kufanya mambo yafuatayo:

i. Kuimarisha taratibu za kuainisha maeneo muhimu ya kitaifa ya kipaumbele na kimkakati yanayohitaji fursa za ufadhili wa masomo ndani na nje ya nchi;

ii. Kuimarisha taratibu za upatikanaji wa taarifa na matangazo ya fursa za ufadhili wa masomo ndani na nje ya nchi;

iii. Kukuza ushirikiano na taasisi na wadau mbalimbali ikiwemo Balozi za ndani na nje ya nchi, taasisi za umma na binafsi;

iv. Kujenga uwezo wa waratibu na wasimamizi wa fursa za ufadhili wa masomo ndani na nje ya nchi katika ofisi na taasisi mbali mbali ikiwemo WyEST, taasisi za elimu, taasisi za uwakala wa elimu, taasisi za dini na binafsi ili kuboresha ufanisi;

v. Kujenga uwezo kwa wanaotafuta na kufanya maombi ya fursa za ufadhili wa masomo ndani na nje ya nchi ikiwemo wanafunzi na wazazi;

vi. Kuweka mifumo ya uratibu, upatikanaji, kuongezeka kwa idadi, usimamizi na ufuatiliaji wa fursa za ufadhili wa masomo ndani na nje ya nchi;

vii. Kutenga bajeti kwa ajili ya utekelezaji wa programu za kujenga uwezo; na

viii. Kufanya ufuatiliaji na tathmini ili kubaini mafanikio na changamoto zilizomo ndani ya fursa za ufadhili wa masomo ndani na nje ya nchi.

## 1.7 Muundo wa Mwongozo

Mwongozo huu una sura nne. Sura ya Kwanza ambayo ni utangulizi inajumuisha usuli, umuhimu na malengo ya mwongozo. Sura ya Pili imejikita kwenye utaratibu wa

kuongeza fursa za ufadhili wa masomo ndani na nje ya nchi. Sura ya Tatu inaelezea kuhusu majukumu ya Serikali, taasisi za umma na binafsi. Sura ya Nne inahusu ufuatiliaji na tathmini pamoja na mpango kazi wa mwongozo.

## 1.8 Utaratibu wa Kuandaa Mwongozo

Mwongozo umeandaliwa kupitia mchakato wa kina wa kutafakari na mashauriano mbalimbali. Aidha, mbinu mbalimbali zilitumika kuandaa Mwongozo huu wa kuongeza fursa za ufadhili wa masomo ndani na nje ya nchi ikiwemo kupitia nyaraka mbalimbali na kuhusisha na kukusanya maoni mbalimbali.

### 1.8.1 Mapitio ya Nyaraka

Njia hii ilihusisha kupitia nyaraka, miongozo, makubaliano na taarifa mbalimbali za elimu nchini, kikanda na kimataifa inayoainisha umuhimu, uhitaji na uratibu wa fursa za ufadhili wa masomo ndani na nje ya nchi. Nyaraka zilizopitiwa za kitaifa ni pamoja na sera ya elimu, kitabu cha mwongozo cha Tume ya vyuo vikuu Tanzania, sera ya umataifishaji ya Chuo Kikuu cha Dar es Salaam na sera ya umataifishaji ya Chuo Kikuu cha Dodoma, Ilani ya Chama cha Mapinduzi (CCM) na *Science, Technology and Innovation Strategy for Africa* (STISA).

### 1.8.2 Kukusanya Maoni ya Wadau

Maoni kutoka kwa wadau mbalimbali wa elimu wa kitaifa, kikanda na kimataifa yalikusanywa, kufanyiwa uchambuzi na kutumika kwenye uandaaji wa mwongozo huu. Utaratibu wa ukusanyaji wa maoni ulihusisha warsha na wadau kutoka taasisi za elimu, taasisi za uwakala wa elimu, taasisi rekebu za elimu (TCU na NACTVET), baraza la mitihani (NECTA), Chama cha wamiliki wa shule binafsi, Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali-Zanzibar, Wizara ya mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi, Umoja wa Wanafunzi wa Vyuo Vikuu (TAHILISO), Mabaraza ya Kitaaluma, na Umoja wa Vyuo Vikuu ya Umma na Binafsi.

## 1.9 Walengwa

Mwongozo huu umetengenezwa kufaa wadau wote katika mnyororo wa utoaji, uratibu mpaka utumiaji wa mwisho wa fursa za ufadhili wa masomo ndani na nje ya nchi. Wadau hawa ni pamoja na nchi na taasisi mbalimbali zinazotoa fursa za ufadhili; serikali, balozi na taasisi za umma, taasisi binafsi na za kidini zinazopokea na kuratibu fursa hizi, wazazi, walezi na wanafunzi wanaotafuta fursa hizi kwa ajili ya kupata ufadhili wa masomo ndani na nje ya nchi.

# SURA YA PILI

## 2. UTARATIBU WA KUONGEZA FURSA ZA UFADHILI WA MASOMO NDANI NA NJE YA NCHI

Malengo ya Serikali ni kuongeza fursa za ufadhili wa masomo ndani na nje ya nchi. Ili kutimiza malengo hayo, ni muhimu kuwepo kwa utaratibu wa kuongeza upatikanaji wa fursa za masomo ndani na nje ya nchi. Mwongozo huu umeweka taratibu mbalimbali za upatikanaji wa fursa za ufadhili wa masomo ndani na nje ya nchi pamoja na kujenga uwezo kwa wadau mbalimbali kuhusu upatikanaji wa fursa.

Aidha mwongozo huu ni mahususi kwa fursa za ufadhili wa masomo kwa watanzania kabla ya kupata ajira ya umma (pre-service). Waliopo kwenye ajira wataongozwa na utaratibu wa Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora.

### 2.1 Fursa za Ufadhili wa Masomo Ndani na Nje ya Nchi

Fursa za ufadhili wa masomo ndani na nje ya nchi zinahusu uwezekano wa kupata msaada wa kifedha kwa ajili ya wanafunzi, watafiti, au wataalamu kusoma katika taasisi za elimu zilizopo ndani na nje ya nchi.

Fursa hizi hutoa njia bora za kuendeleza elimu, tafiti na maendeleo ya kitaaluma kwenye nyanja mbalimbali. Ufadhili huu unaweza kutolewa na serikali,watu binafsi, mashirika yasiyo ya kiserikali, mashirika ya kimataifa, taasisi za dini au hata sekta binafsi.

#### 2.1.1 Madhumuni ya Ufadhili wa Masomo Ndani na Nje ya Nchi

i. **Kuongeza ujuzi na maarifa**: Fursa hizi zinatoa nafasi ya wanafunzi kujiendeleza kitaaluma kwa kusoma kwenye taasisi ambazo zina umahiri wa hali ya juu katika nyanja husika. Jambo hili litasaidia nchi kuwa na wataalamu wenye ujuzi na maarifa ya kiwango cha juu yatakayokidhi mahitaji ya wananchi wake.

ii. **Kujenga mahusiano ya kimataifa**: Wanafunzi wanaosoma nje ya nchi wanapata nafasi ya kujifunza tamaduni na mitazamo mipya ya kimataifa, hivyo kuimarisha ushirikiano kati ya nchi na nchi.

iii. **Kukuza eneo la utafiti na ubunifu**: Ufadhili wa masomo ndani na nje ya nchi unawezesha kushiriki kwenye miradi ya kiutafiti na kiuvumbuzi katika nyanja tofauti ambazo zinaweza kuwa na manufaa kwa nchi husika.

iv. **Kuendeleza wataalamu wa kisekta**: Nchi zinazohitaji wataalamu katika sekta fulani kama vile teknolojia, afya, nishati au kilimo, huweka kipaumbele cha kupeleka wanafunzi kusomea sekta hizo ili kuleta maarifa yaliyoboreshwa nchini mwao.

### 2.1.2 Aina za Fursa za Ufadhili wa Masomo Ndani na Nje ya Nchi

i. **Ufadhili kamili**: Hii ni aina ya ufadhili ambapo mwanafunzi anapata msaada wa kifedha unaohusu gharama zote za masomo, malazi, chakula, na gharama nyingine za kimaisha. Mfano wa ufadhili kamili ni ule unaotolewa na mashirika ya kimataifa kama vile DAAD (Ujerumani), Chevening (Uingereza), au Fulbright (Marekani).

ii. **Ufadhili wa sehemu**: Ufadhili huu unahusu kulipiwa sehemu ya gharama kama vile ada za masomo pekee au malazi. Huu unaweza kutolewa na mashirika binafsi au taasisi za kidini.

iii. **Ufadhili wa utafiti**: Ufadhili wa aina hii hutolewa kwa watafiti au wanafunzi wa shahada ya umahiri na uzamivu ili kufadhili miradi ya utafiti wa kisayansi na kitaaluma. Kwa mfano fursa zinazotolewa na taasisi kama UNESCO au Benki ya Dunia kwa ajili ya utafiti.

iv. **Ufadhili wa masomo ya maendeleo**: Hizi ni fursa zinazotolewa na nchi au mashirika yanayolenga kuimarisha uwezo wa wataalamu kutoka nchi zinazoendelea. Kwa mfano ufadhili unaotolewa na Nchi za Jumuiya ya Madola (Commonwealth).

### 2.1.3 Namna ya Kupata Fursa za Ufadhili wa Masomo Ndani na Nje ya Nchi

i. Kutafuta taarifa: Ni muhimu kufuatilia taarifa kupitia tovuti za mashirika yanayotoa ufadhili, taasisi za elimu na vyuo vikuu vya kimataifa.

ii. Maombi na masharti: Kila ufadhili una masharti yake, hivyo ni muhimu kuelewa vigezo, nyaraka zinazohitajika na mwisho wa muda wa maombi.

iii. Kujitayarisha vizuri: Waombaji wanapaswa kuwa na maandiko bora ya kuonyesha motisha na malengo yao kitaaluma, pamoja na maandalizi mazuri ya nyaraka kama vile barua za mapendekezo na vyeti vya kitaaluma.

## 2.2 Mahitaji ya Fursa za Ufadhili wa Masomo Ndani na Nje ya Nchi

Ili kubainisha mahitaji kwa ajili ya kupata fursa za ufadhili wa masomo ndani na nje ya nchi, ni muhimu kufuata hatua zifuatazo:

### 2.2.1 Kubainisha Maeneo na Fani za Kimkakati ya Nchi kwa Ajili ya Kutafuta Ufadhili wa Masomo Ndani na Nje ya Nchi

i. Kuangalia dira ya maendeleo ya nchi, mipango ya kimkakati, na sera za elimu ili kubainisha fani zinazochangia kwa kiasi kikubwa maendeleo ya kiuchumi, kijamii na kiteknolojia.

ii. Kutathmini sekta zinazohitaji ujuzi maalumu kama vile afya, uhandisi, kilimo, mazingira, nishati, TEHAMA, na teknolojia ya kisasa, ambazo zinaweza kuchochea maendeleo endelevu.

iii. Kufanya mashauriano na taasisi mbalimbali kama vile wizara husika na vyuo vikuu ili kupata maoni kuhusu fani ambazo ni kipaumbele cha kitaifa.

### 2.2.2 Kubainisha Nchi Hisani Zenye Umahiri katika Fani za Kimkakati Zinazohitajika Nchini kwa Ajili ya Ufadhili wa Masomo

i. Kuchunguza nchi ambazo zimejikita na zina umahiri wa kipekee katika fani zilizobainishwa kimkakati kwa maendeleo ya taifa.

ii. Kuangalia historia ya nchi hizo katika kutoa mafunzo bora, utafiti wa hali ya juu, na programu za ufadhili zinazolenga wanafunzi wa kimataifa, hasa kutoka nchi zinazoendelea.

iii. Kujenga ushirikiano wa kimkakati na nchi hizo kupitia balozi zao, mashirika ya misaada, na taasisi za elimu ili kupata taarifa za fursa za ufadhili.

### 2.2.3 Kubainisha Maeneo ya Ushirikiano Ambayo Taasisi za Elimu, Dini na Mashirika Yasiyo ya Kiserikali Yanapata au Kutoa Ufadhili wa Masomo Ndani na Nje ya Nchi

i. Kutafuta taarifa kutoka taasisi za elimu, dini, na Mashirika yasiyo ya Serikali ambazo zinajihusisha na kutoa au kuratibu ufadhili wa masomo ndani na nje ya nchi.

ii. Kushirikiana na taasisi hizo ili kubaini aina za ufadhili zinazotolewa, kama vile masomo ya muda mfupi, utafiti, au mafunzo ya juu, na nchi zinazopokea au kutoa fursa hizo.

iii. Kutumia mitandao ya kijamii, tovuti rasmi, na majukwaa ya habari kupata taarifa kuhusu mashirika na taasisi zinazotoa ufadhili wa kimataifa.

### 2.2.4 Kubainisha Fani Ambazo kwa Umuhimu na Unyeti Wake, Serikali Itawafadhili Watanzania Kusoma Ndani na Nje ya Nchi

i. Kushirikiana na Serikali, kupitia wizara husika kama vile Wizara ya Elimu, Wizara ya Afya, na Wizara ya Nishati, kubainisha fani ambazo ni muhimu kwa maendeleo ya kitaifa na ambazo zitaongeza ujuzi wa kitaalamu.

ii. Kutathmini maeneo yanayohitaji wataalamu wa hali ya juu kutokana na upungufu wa wataalamu wa ndani, na maeneo yanayoathiri moja kwa moja ustawi wa taifa kama vile afya ya umma, usalama wa chakula, na nishati mbadala.

iii. Kutoa mapendekezo kwa Serikali kuhusu mikakati ya muda mfupi na mrefu ya kuwafadhili wanafunzi wanaochukua fani hizo ndani na nje ya nchi kwa maslahi ya taifa.

## 2.3 Kubainisha Fursa za Ufadhili wa Masomo Ndani na Nje ya Nchi

### 2.3.1 Ushirikiano

i. Kuanzisha ushirikiano baina ya Serikali, mashirika, na taasisi za elimu za nchi, mashirika, au taasisi za ndani na nje zinazotoa ufadhili wa masomo.

ii. Kuweka utaratibu wa kuimarisha mawasiliano na mahusiano na nchi, mashirika, au taasisi za nje ambazo tumeingia nazo makubaliano au mikataba ya ushirikiano.

### 2.3.2 Balozi za Ndani na Nje ya Nchi

i. Kuimarisha uratibu wa fursa za ufadhili wa masomo ndani na nje ya nchi kwa kuwa na waambata elimu hususan katika balozi za Tanzania zilizopo katika nchi za kimkakati;

ii. Balozi kuwa vyanzo muhimu vya taarifa kuhusu fursa na programu za ufadhili zinazotolewa na serikali na mashirika katika nchi hizo; na

iii. Kusaidia katika kuunganisha, kutoa huduma muhimu na taarifa za wanafunzi wanaopata fursa na kushiriki programu za ufadhili wa masomo ndani na nje ya nchi.

### 2.3.3 Taasisi za Uwakala wa Elimu

i. Kushiriki katika kutafuta fursa za ufadhili wa masomo ndani na nje ya nchi;

ii. Kushiriki kutoa mafunzo na kujenga uwezo wa kufanya maombi ya fursa za ufadhili wa masomo ndani na nje ya nchi; na

iii. Kuboresha utendaji na kuweka uaminifu wa upatikanaji, usambazaji na uratibu wa fursa za ufadhili wa masomo ndani na nje ya nchi.

### 2.3.4 Watanzania Waishio Nje ya Nchi (Diaspora)

i. Kusaidia kwa kushirikisha taarifa kuhusu fursa mpya za ufadhili, vigezo vya kuomba ufadhili, na tarehe muhimu za maombi na kuwa mabalozi wa fursa za masomo zinazopatikana katika nchi wanazoishi;

ii. Kujenga mtandao wa kimawasiliano ili kuunganisha wanafunzi wa Tanzania na taasisi au mashirika yanayotoa ufadhili wa masomo ndani na nje ya nchi;

iii. Kuanzisha au kukuza mahusiano na vyuo vikuu na mashirika ya elimu kwa kushirikiana nao kutafuta fursa za masomo;

iv. Kushiriki katika kujenga uwezo kwa waombaji hususan kwa waiofanikiwa kupata ufadhili wa masomo kwa kuwa washauri wa wanafunzi wa Tanzania, wakiwaelekeza jinsi ya kuandika maombi bora ya ufadhili, kujiandaa na usaili, na jinsi ya kujiandaa kimahesabu na kitaaluma;

v. Kushirikiana na wadau kama vile serikali, balozi, taasisi za elimu na makampuni binafsi katika kuanzisha programu maalumu za ufadhili wa masomo kwa wanafunzi wa Kitanzania; na

vi. Kuanzisha au kuchangia kwenye mfuko wa ufadhili wa masomo kwa wanafunzi wa Kitanzania kusoma ndani na nje ya nchi kwa kushirikiana na mashirika ya kimataifa au serikali zao kusaidia elimu ya Watanzania.

#### 2.3.5 Makampuni, Wafanyabiashara, Mashirika ya Dini na Watu Binafsi

i. Makampuni, wafanyabiashara, Mashirika ya Dini na watu binafsi kutoa fursa za ufadhili wa masomo ndani na nje ya nchi; na

ii. Serikali kuweka utaratibu wa kushawishi na kutambua makampuni, wafanyabiashara na watu binafsi wanaotoa fursa za ufadhili wa masomo ndani na nje ya nchi.

#### 2.3.6 Viongozi wa Serikali

i. Serikali kutoa waraka maalumu wa kuhamasisha viongozi wa serikali na watendaji wa ngazi za juu kushiriki kikamilifu katika kutafuta fursa za ufadhili wa masomo katika sekta mbalimbali, hasa wanaposafiri kwenda nje ya nchi kwa shughuli rasmi; na

ii. Serikali kuweka utaratibu wa kushawishi na kuwatambua viongozi wa serikali na watendaji wa ngazi za juu wanaoshiriki kikamilifu kutafuta fursa za ufadhili wa masomo ndani na nje ya nchi.

### 2.4 Kutangaza Fursa za Ufadhili wa Masomo Ndani na Nje ya Nchi

Ili kutanua wigo wa fursa za ufadhili wa masomo ndani na nje ya nchi kuweza kuwafikia watanzania wengi zaidi, kwa njia rahisi na kwa uwazi mwongozo huu unatoa taratibu zifuatazo:

#### 2.4.1 Kuboresha Njia za Kutangaza Fursa za Ufadhili

i. Kuhakikisha kuwa taarifa za ufadhili wa masomo zinatangazwa kupitia vyombo mbalimbali vya habari, kama vile redio, televisheni, magazeti, na mitandao ya kijamii kama Facebook, Twitter, Instagram, na LinkedIn; na

ii. Kutoa taarifa za ufadhili wa masomo kupitia taasisi za elimu kama vile shule, vyuo vikuu, na vituo vya mafunzo.

### 2.4.2 Kushiriki na Kuandaa Makongamano na Maonesho

i. Kushiriki katika maonesho na makongamano ya kitaaluma yanayohusisha elimu na ufadhili. Hii inaweza kutoa nafasi ya moja kwa moja kwa washiriki kuuliza maswali na kupata taarifa sahihi kuhusu fursa za ufadhili wa masomo ndani na nje ya nchi; na

ii. Wizara ya Elimu kwa kushirikiana na wadau mbalimbali wa sekta ya elimu kuandaa maonesho ya elimu ya kimataifa yanayolenga kutangaza fursa za masomo ndani na nje ya nchi.

### 2.4.3 Ukurasa Mahususi wa Fursa za Ufadhili wa Masomo Ndani na Nje ya Nchi

i. Kutengeneza ukurasa maalumu unaopatikana kwenye tovuti ya Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia ambao utahifadhi taarifa zote muhimu kuhusu fursa za ufadhili wa masomo nje ya nchi. Huu ukurasa uwe rahisi kupatikana, kusomwa na uwe wenye taarifa zinazohuishwa mara kwa mara; na

ii. Ukurasa maalumu wa fursa za masomo nje ya nchi ujumuishe taarifa za kina kuhusu jinsi ya kuomba fursa hizo, vigezo vya kuchaguliwa, na muda wa mwisho wa kuomba.

### 2.4.4 Jumuiya na Mashirika ya Kijamii

i. Kushirikiana na jumuiya za kijamii kama vile vikundi vya elimu, vikundi vya kijamii vya wanafunzi wa zamani (alumni), na vyama vya kitaaluma kusambaza taarifa za ufadhili wa masomo ndani na nje ya nchi. Vyama vya wanafunzi, vyama vya walimu na wakufunzi pia vinaweza kutumika katika usambazaji wa taarifa hizi; na

ii. Kushirikiana na mashirika yasiyo ya kiserikali yanayohusika na elimu na maendeleo katika kusambaza fursa za masomo ndani na nje ya nchi. Haya mashirika yanaweza kushirikiana na Wizara ya Elimu au taasisi za elimu katika kuandaa vipindi maalumu vya kuwafahamisha wananchi juu ya fursa hizi.

## 2.5 Usimamizi wa Fursa za Ufadhili wa Masomo Ndani na Nje ya Nchi

Ili kuongeza ushirikiano, uwazi, na ufanisi katika usimamizi wa fursa za ufadhili wa masomo ndani na nje ya nchi kwa watanzania, huku ukilinda maslahi ya taifa, mwongozo huu unatoa utaratibu ufuatao:

### 2.5.1 Dawati Maalumu kwa Ajili ya Usimamizi wa Fursa za Ufadhili wa Masomo Ndani na Nje ya Nchi

Kuanzisha dawati maalumu ndani ya Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia (WyEST) linalosimamia na kuratibu fursa zote za ufadhili wa masomo ndani na nje ya nchi.

### 2.5.2 Uhakiki na Uidhinishaji wa Fursa

i. Kuweka utaratibu maalumu wa uhakiki na uidhinishaji wa aina za ufadhili wa masomo ikiwemo uhakiki wa vigezo vya ufadhili, masharti yanayohitajika, maeneo ya masomo, na tafiti zinazohusika; na

ii. Kushirikisha mamlaka husika kama vile COSTECH, wizara za elimu, na wizara ya mambo ya ndani ili kulinda maslahi na usalama wa taifa.

### 2.5.3 Kupokea Fursa na Kuongeza Uelewa

i. Kuweka utaratibu wa kupokea fursa za ufadhili kutoka kwenye nchi, taasisi na mashirika mbalimbali; na

ii. Kuhakikisha fursa hizi zinawafikia wanafunzi na watanzania kwa urahisi kupitia kampeni za uhamasishaji na kuongeza uelewa wa mahitaji na vipengele vya ufadhili.

### 2.5.4 Taasisi za Wakala wa Elimu

Kuweka mfumo wa ushirikiano na taasisi za uwakala wa elimu nchini ili kusaidia kuratibu na kusimamia fursa za ufadhili wa masomo ndani na nje ya nchi na kuwezesha ufadhili kufikiwa na wanafunzi kwa urahisi zaidi.

### 2.5.5 Mfumo wa Taarifa na Mrejesho

i. Kuweka mfumo wa kuhifadhi na kuratibu taarifa za watanzania wanaoenda masomoni nje ya nchi, wanaorudi, na wale ambao bado hawajarudi; na

ii. Kutoa taarifa ya ufuatiliaji wa mafanikio ya fursa na programu za ufadhili na kupima faida na athari zake kwa jamii.

### 2.5.6 Kuunganisha Mifumo ya Kidijitali

i. Kuweka mfumo wa kidijiti unaounganisha taarifa za fursa za ufadhili na wanufaika, ikijumuisha programu zinazotolewa, muda wa masomo, na matokeo ya wanafunzi;

ii. Mfumo huu utaongeza ufanisi wa kufuatilia maendeleo ya wanafunzi na kusaidia katika upangaji wa sera za ufadhili; na

iii. Kuratibu vikao vya mara kwa mara kati ya sekta husika kama vile uhamiaji, WyEST, na Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki ili kuhakikisha kuwa mifumo ya usimamizi wa ufadhili inaendelea kuboreshwa kwa lengo la kuongeza ufanisi.

## 2.6 Kujenga Uwezo

### 2.6.1 Waombaji wa Ufadhili wa Masomo Ndani na Nje ya Nchi

i. Kuweka utaratibu maalumu wa kutoa mafunzo kwa umma kuhusu fursa zinazopatikana za ufadhili wa masomo ndani na nje ya nchi. Mafunzo haya yatatolewa kwa njia ya semina, warsha, mafunzo ya mtandaoni, na makongamano ili kuwaelimisha wanafunzi, wazazi, na wadau wengine juu ya mbinu za kuandika maombi bora ya ufadhili;

ii. Kuunda majukwaa ya usajili ambapo waombaji wanaweza kupata taarifa, ushauri, na msaada wa kuandaa nyaraka muhimu kama barua za maombi, wasifu wa kitaaluma (CV), na nyaraka za kiakademia zinazohitajika kwa maombi;

iii. Kutoa mafunzo na kampeni za uhamasishaji mahususi kwa wazazi ili kuhakikisha wanapata uelewa wa jinsi wanavyoweza kusaidia watoto wao katika mchakato wa maombi ya ufadhili; na

iv. Kuhamasisha wazazi kuwa mstari wa mbele katika kuwawezesha watoto wao kifedha, kiakili na kuwajenga kimaadili ili wawe na motisha ya kufanya maombi ya masomo ndani na nje ya nchi na kufanikiwa.

### 2.6.2 Waratibu wa Fursa za Ufadhili wa Masomo Ndani na Nje ya Nchi

i. Kutoa mafunzo ya uratibu wa mafunzo ya kujenga uwezo wa usimamizi na uratibu wa fursa za ufadhili wa masomo ndani na nje ya nchi;

ii. Kujenga uwezo wa utumiaji wa mifumo, kurasa za tovuti katika kuhakikisha taarifa muhimu za fursa za ufadhili zinapatikana na kuwekwa wazi kwa usahihi; na

iii. Kujengewa uwezo wa diplomasia ya elimu na fursa zinazohusiana na elimu ili kuwezesha ujuzi wa kubaini mahitaji ya kitaifa katika utandawazi, pamoja na kutafuta fursa za ufadhili wa masomo ndani na nje ya nchi.

# SURA YA TATU

## 3. MAJUKUMU

Ili kufanikisha mwongozo wa kuongeza fursa za ufadhili wa masomo ndani na nje ya nchi, wadau mbalimbali watahusika. Hivyo, sura hii inaeleza majukumu na uwajibikaji.

### 3.1 Majukumu ya Serikali

Pamoja na usimamizi wa jumla wa utekelezaji wa Mwongozo huu, Serikali kupitia Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojioa, itatekeleza majukumu yafuatayo:

i. Kushirikiana na Wizara za kisekta kubaini maeneo na fani za kimkakati za nchi kwa ajili ya kupata ufadhili wa masomo ndani na nje ya nchi;

ii. Kubaini nchi hisani zenye umahiri katika fani za kimkakati zinazohitajika nchini kwa ajili ya ufadhili wa masomo;

iii. Kuimarisha mawasiliano na ushirikiano wa kimkakati kati ya Wizara na Balozi za Tanzania katika nchi mbalimbali kupitia Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki;

iv. Kubaini fursa za ufadhili wa masomo ndani na nje ya nchi;

v. Kuweka utaratibu wa kutangaza fursa za masomo ndani na nje ya nchi;

vi. Kuratibu upatikanaji wa nyaraka mbalimbali zinazohitajika kwa ajili ya fursa za masomo ndani na nje ya nchi;

vii. Kujenga uwezo wa kusimamia na upatikanaji wa fursa za ufadhili wa masomo ndani na nje ya nchi;

viii. Kuthibiti Taasisi za uwakala wa fursa za masomo ndani na nje ya nchi kwa kuimarisha utekelezaji wa kanuni na mwongozo wa usajili wa taasisi hizo na majukumu yao iliyotengenezwa na Tume ya Vyuo Vikuu nchini (TCU);

ix. Kuhakiki na kuidhinisha aina za ufadhili, maeneo ya ufadhili, maeneo ya tafiti zinazohusika na ufadhili ili kulinda maslahi na usalama wa Taifa. Hapa dawati la ufadhili litafanya kazi kwa ukaribu na taasisi za elimu, tafiti, na COSTECH; na

x. Kusimamia utekelezaji wa mwongozo wa kuongeza fursa za ufadhili wa masomo ndani na nje ya nchi.

### 3.2 Majukumu ya Balozi

Katika kutekeleza mwongozo wa kuongeza fursa za ufadhili wa masomo ndani na nje ya nchi, Balozi zitatekeleza majukumu yafuatayo:

i. Kubaini fursa za ufadhili wa masomo ndani na nje ya nchi na kuziwasilisha serikalini kupitia taratibu za kiserikali;

ii. Kuratibu na kusimamia upatikanaji wa taarifa za wanufaika wa ufadhili wa masomo katika nchi wanazoiwakilisha Tanzania; na

iii. Kutoa usaidizi kwa wanufaika wa ufadhili wa masomo ndani na nje ya nchi katika masuala ya kijamii na kiutamaduni.

## 3.3 Majukumu ya Taasisi za Elimu

i. Kubaini fursa za ufadhili wa masomo ndani na nje ya nchi;

ii. Kuratibu na kusimamia fursa za ufadhili wa masomo ndani na nje ya nchi; na

iii. Kutoa taarifa za wanufaika wa ufadhili wa masomo ndani na nje ya nchi.

## 3.4 Majukumu ya Taasisi za Uwakala wa Elimu

i. Kubaini fursa za ufadhili wa masomo ndani na nje ya nchi;

ii. Kuujulisha umma wa Tanzania juu ya uwepo wa fursa za ufadhili wa masomo ndani na nje ya nchi;

iii. Kuandaa taarifa za ufadhili wa masomo ndani na nje ya nchi ambazo zimeratibiwa na mawakala na kuwasilishwa Wizarani;

iv. Kuzingatia na kufuata kanuni na mwongozo wa usajili wa Taasisi za Uwakala iliyotengenezwa na Tume ya Vyuo Vikuu nchini (TCU) na

v. Kuimarisha ushirikiano baina ya taasisi na WyEST katika uratibu wa fursa za masomo.

# SURA YA NNE

## 4. UFUATILIAJI NA TATHMINI

Ili kufanikisha utekelezaji wa Mwongozo wa kuongeza fursa za ufadhili wa masomo ndani na nje ya nchi, ni muhimu kuweka mfumo na utaratibu wa ufuatiliaji na tathmini. Lengo la ufuatiliaji na tathmini ni kuhakikisha kuwa malengo ya Mwongozo yaliyokusudiwa yanafikiwa na changamoto za utekelezaji zinajulikana na kutatuliwa kwa wakati.

Ufuatiliaji na tathmini zitafanyika katika ngazi mbalimbali za utekelezaji wa Mwongozo kila mwaka kulingana na viashiria kama ilivyoainishwa kwenye jedwali la utekelezaji, ufuatiliaji na tathmini ya mwongozo wa kuongeza fursa za ufadhili wa masomo ndani na nje ya nchi (Jedwali Na. 1).

Taarifa ya ufuatiliaji na tathmini itatumika katika kuijulisha Wizara na wadau husika kwa ajili ya maboresho ya Mwongozo.

## Jedwali Na. 1: JEDWALI LA UTEKELEZAJI, UFUATILIAJI NA TATHMINI YA MWONGOZO WA KUONGEZA FURSA ZA UFADHILI WA MASOMO NDANI NA NJE YA NCHI

| | MKAKATI WA KUFANIKISHA MWONGOZO | VIASHIRIA VYA UTEKELEZAJI | KIPINDI CHA UTEKELEZAJI | WAHUSIKA |
|---|---|---|---|---|
| **KUBAINISHA MAHITAJI YA FURSA** | | | | |
| 1.1 | Kubainisha mahitaji ya maeneo na fani za kipaumbele. | Uwepo wa orodha ya maeneo na fani za kimahitaji. | Aprili kila mwaka. | WyEST |
| 1.2 | Kubainisha nchi zenye umahiri katika maeneo ya mahitaji na kipaumbele. | Uwepo wa orodha ya nchi hisani . | Aprili 2026 | WyEST |
| 1.3 | Maeneo ya ushirikiano. | Uwepo wa taarifa ya maeneo ya ushirikiano kwa fursa za maeneo ya mahitaji. | Aprili 2026 | WyEST |
| 1.4 | Kubaini fani za umuhimu na unyeti. | Uwepo wa taarifa ya fani za umuhimu na unyeti. | Aprili 2026 | WyEST |
| **KUBAINISHA FURSA ZA UFADHILI WA MASOMO NDANI NA NJE YA NCHI** | | | | |
| **2.1** | **BALOZI ZA TANZANIA NJE YA NCHI** | | | |
| 2.1.1 | Balozi kuingia makubaliano na nchi au taasisi husika katika kutoa ufadhili wa masomo ndani na nje ya nchi. | Mikataba ya makubaliano. | Juni 2026 (Endelevu) | Ofisi za ubalozi, na Wizara ya mambo ya nje na ushirikiano wa Afrika Mashariki |
| 2.1.2 | Balozi zetu kuratibu mahusiano kati ya taasisi za elimu za ndani na nje ya nchi hususan yanayolenga fursa za ufadhili. | Mfumo wa kuratibu mahusiano.<br><br>Idadi ya mahusiano yaliyoratibiwa. | Juni 2026<br><br>Juni kila mwaka | Ofisi za ubalozi, Taasisi za elimu, Wizara ya mambo ya nje na WyEST |
| 2.1.3 | Kujenga mahusiano na taasisi katika nchi za kimkakati ili kutafuta fursa za ufadhili wa masomo. | Idadi ya Taasisi zilizoainishwa na Taarifa ya Utekelezaji. | Mei 2026 (endelevu) | Ofisi za ubalozi, Taasisi nchini na WyEST |

| | MKAKATI WA KUFANIKISHA MWONGOZO | VIASHIRIA VYA UTEKELEZAJI | KIPINDI CHA UTEKELEZAJI | WAHUSIKA |
|---|---|---|---|---|
| 2.1.4 | Balozi kujenga na kuimarisha mahusiano na wizara za nchi wenyeji ili kupata fursa zaidi za ufadhili wa masomo kwa watanzania kusoma ndani na nje ya nchi. | Taarifa ya Utekelezaji na Idadi ya Taasisi zilizopo. | Juni 2026 | Ofisi za ubalozi na Wizara ya mambo ya Nje na ushirikiano wa Afrika Mashariki |
| 2.1.5 | Kuomba nafasi za ufadhili wa masomo kupitia Balozi zetu katika nchi husika. | Taarifa ya utekelezaji na idadi ya maombi yaliyopelekwa. | Mei 2026 | WyEST |
| 2.1.6 | Balozi kuwa na waambata elimu katika nchi za kimkakati katika Balozi za Tanzania nchi za nje watakaoratibu fursa za ufadhili wa masomo kwa watanzania kusoma ndani na nje ya nchi. | Idadi ya nchi za kimkakati zilizo ainishwa na taarifa utekelezaji. | 2025/2026 | Wizara ya Mambo ya nje na ushirikiano wa Afrika Mashariki na WyEST |
| 2.1.7 | Balozi kushirikiana na taasisi za uwakala wa elimu katika kutafuta fursa za ufadhili wa masomo ndani na nje ya nchi. | Taarifa ya utekelezaji. | 2025/2026 | Ofisi za Ubalozi, Taasisi za Uwakala wa elimu na WyEST |
| 2.1.8 | Balozi kushirikiana na diaspora katika kutafuta fursa za ufadhili wa masomo ndani na nje ya nchi. | Taarifa ya utekelezaji. | 2025/2026 | Ofisi za ubalozi na WyEST |
| **2.2** | **BALOZI ZA NCHI ZA NJE** | | | |
| 2.2.1 | Kushirikiana na Balozi za nje kuainisha fursa na maeneo ya ufadhili yanayopatikana katika nchi zao. | Orodha ya fursa zilizopo katika nchi husika. | 2025/2026 | WyEST na Wizara ya Mambo ya nje na ushirikiano wa Afrika Mashariki |
| 2.2.2 | Kuwasilisha maeneo ya kimkakati ya nchi kwenye Balozi za nje kwa ajili ya kupata ufadhili wa masomo ndani na nje ya nchi. | Kuainishwa maeneo ya kimkakati. Kuwasilisha andiko kuhusu maeneo ya kimkakati yanayohitaji ufadhili kwenye ofisi za balozi. | Desemba 2025 | WyEST na Wizara ya Mambo ya nje na ushirikiano wa Afrika Mashariki |

| | MKAKATI WA KUFANIKISHA MWONGOZO | VIASHIRIA VYA UTEKELEZAJI | KIPINDI CHA UTEKELEZAJI | WAHUSIKA |
|---|---|---|---|---|
| 2.2.3 | Kutumia Balozi za nje kuunganisha taasisi nchini na taasisi za nje ya nchi ili kupata fursa za ufadhili wa masomo ndani na nje ya nchi. | Idadi ya mikataba iliyosainiwa.<br>Fursa za ufadhili zinazopatikana kutoka taasisi za ndani na nje. | Desemba 2025 (endelevu kila mwaka) | Taasisi nchini, Ofisi za balozi na WyEST |
| 2.2.4 | Taasisi za elimu, shule na vyuo kuingia makubaliano na Balozi ili kupata fursa za ufadhili wa wafanyakazi, watafiti na wanafunzi kwenda kusoma kwa muda mfupi au muda mrefu ndani na nje ya nchi. | Idadi ya mikataba ya makubaliano iliyosainiwa. | Juni 2026 (endelevu kila mwaka) | Taasisi za elimu nchini, Ofisi za balozi na WyEST |
| 2.2.5 | Kuainisha na kutangaza fursa za ufadhili wa masomo zinazotolewa na kuratibiwa moja kwa moja na ofisi za Balozi mbalimbali zilizoko hapa nchini. | Orodha ya fursa za ufadhili wa masomo kwa kila nchi.<br><br>Mkakati wa kutangaza fursa hizo kila mwaka. | Disemba 2025 (itaboreshwa kila mwaka) | Ofisi za ubalozi na WyEST |
| 2.2.6 | Kushirikisha Balozi za nje kwenye makongamano na maonesho ya kitaaluma na utafiti yanayoandaliwa na taasisi za elimu nchini. | Kuandaa ratiba ya makongamano na maonyesho ya kitaaluma.<br><br>Kupeleka mwaliko kwa balozi kushiriki. | Novemba 2025<br><br>Disemba 2025 (Endelevu) | WyEST na Taasisi husika (TCU, NACTIVET) |
| **2.3** | **MAKUBALIANO YA KITAIFA NA NCHI HISANI** | | | |
| 2.3.1 | Kubainisha fani za kimkakati zinazohitajika nchini kwa ajili ya kujenga uwezo kupitia ufadhili wa masomo ndani na nje ya nchi. | Idadi ya fani za kimkakati zilizoainishwa. | Oktoba 2025 | WyEST |
| 2.3.2 | Kubainisha nchi hisani zenye umahiri katika fani za kimkakati zinazohitajika nchini kwa ajili ya ufadhili wa masomo. | Orodha ya nchi hisani zenye umahiri na orodha ya fani za kimkakati. | Disemba 2025 (Endelevu) | WyEST |

| | MKAKATI WA KUFANIKISHA MWONGOZO | VIASHIRIA VYA UTEKELEZAJI | KIPINDI CHA UTEKELEZAJI | WAHUSIKA |
|---|---|---|---|---|
| 2.3.3 | Kuingia mikataba ya makubaliano katika masuala ya ufadhili wa masomo ndani na nje ya nchi na nchi ambazo hatuna mikataba nazo. | Idadi ya mikataba ya makubaliano. | Juni 2026 | WyEST |
| 2.3.4 | Kujenga uwezo wa usimamizi na uratibu wa fursa za ufadhili wa masomo ndani na nje ya nchi. | Taarifa ya idadi ya wataalamu waliojengewa uwezo. | Juni 2026 | WyEST |
| 2.3.5 | Kufanya tathmini ya mikataba ya makubaliano ya ufadhili ili kuboresha utekelezaji wa makubaliano. | Taarifa ya Tathmini ya utekelezaji wa mikataba. | Juni 2026 | WyEST |
| **2.4** | **TAASISI ZA ELIMU, DINI, MAKAMPUNI NA MASHIRIKA YASIYO YA KISERIKALI** | | | |
| 2.4.1 | Kubainisha maeneo ya ushirikiano ambayo taasisi za elimu, dini na mashirika yasiyo ya kiserikali yanapata au kutoa ufadhili kwenda kusoma ndani na nje ya nchi. | Kubainisha na kuwepo kwa makubaliano na taasisi za elimu, dini na mashirika yasiyo ya kiserikali juu ya ufadhili. | Juni 2026 | WyEST |
| | | Uwepo na idadi ya maeneo ya ushirikiano katika kupata fursa za ufadhili wa wanafunzi kusoma ndani na nje ya nchi. | Mei, 2026 | WyEST |
| | | Uwepo wa fursa za ufadhili wa masomo zilizobainika. | Mei, 2026 | WyEST |

| | MKAKATI WA KUFANIKISHA MWONGOZO | VIASHIRIA VYA UTEKELEZAJI | KIPINDI CHA UTEKELEZAJI | WAHUSIKA |
|---|---|---|---|---|
| 2.4.2 | Taasisi kuingia mikataba ya makubaliano (MoU) na nchi au washirika mbalimbali ili kuongeza fursa za ufadhili wa masomo ndani na nje ya nchi. | Idadi ya Washirika waliotambulika kuingia mikataba ya makubaliano na Taasisi.<br><br>Uwepo wa mikataba ya makubaliano kati ya Taasisi na Washirika.<br><br>Uwepo wa Fursa za masomo ya ufadhili ndani na nje ya nchi. | Juni 2026<br><br>Mei 2026<br><br>Mei 2026 (endelevu) | Taasisi za Elimu ya Juu |
| 2.4.3 | Kuweka mwongozo wa uratibu wa fursa za ufadhili wa masomo ndani na nje ya nchi. | Uwepo wa mwongozo wa kitaifa wa kuratibu fursa za ufadhili wa masomo zinazopatikana ndani na nje ya nchi.<br><br>Kuandaa mwongozo wa ufadhili wa masomo ndani na nje ya nchi (National Scholarship Framework) ambao utabainisha fursa mbalimbali za ufadhili na kutoa maelekezo kwa wadau wote wanaohusika kupeleka watanzania kusoma nje ya nchi kwa ufadhili binafsi au wa serikali. | Juni 2026 | WyEST. |

| | MKAKATI WA KUFANIKISHA MWONGOZO | VIASHIRIA VYA UTEKELEZAJI | KIPINDI CHA UTEKELEZAJI | WAHUSIKA |
|---|---|---|---|---|
| 2.4.4 | Kubainisha, kuhamasisha na kutambua taasisi na makampuni yasiyo ya kiserikali yenye mchango katika upatikanaji wa fursa za ufadhili wa masomo ndani na nje ya nchi. | Kubainisha taasisi na makampuni yasiyo ya kiserikali katika upatikanaji wa fursa za ufadhili. | Juni 2026 | WyEST |
| | | Kuwepo kwa mpango wa uhamasishaji taasisi na makampuni yasiyo ya kiserikali katika upatikanaji wa fursa za ufadhili. | Juni 2026 | WyEST |
| | | Uwepo wa Fursa za masomo ya ufadhili nje ya nchi kupitia taasisi na makampuni yasiyo ya kiserikali. | Mei 2026 (endelevu) | WyEST |
| **2.5** | **TAASISI ZA UWAKALA WA ELIMU** | | | |
| 2.5.1 | Kuingia makubaliano ya ushirikiano kati ya taasisi za uwakala, wizara na taasisi za elimu kuhusu uratibu wa fursa za ufadhili wa masomo ndani na nje ya nchi. | Idadi ya mikataba ya makubaliano. | Disemba 2025 | Taasisi za Uwakala, Taasisi za Elimu ya Juu na WyEST |
| 2.5.2 | Kuboresha mahusiano kati ya taasisi za uwakala na balozi za ndani na nje ya nchi ili kuongeza fursa za upatikanaji wa ufadhili wa masomo ndani na nje ya nchi. | Idadi ya balozi ndani na nje ya nchi zenye mahusiano na taasisi za uwakala. | Novemba 2025 (endelevu) | Taasisi za Uwakala |
| | | Fursa za masomo zilizopatikana ndani na nje ya nchi. | Juni 2026 (endelevu) | Taasisi za Uwakala |

| | MKAKATI WA KUFANIKISHA MWONGOZO | VIASHIRIA VYA UTEKELEZAJI | KIPINDI CHA UTEKELEZAJI | WAHUSIKA |
|---|---|---|---|---|
| 2.5.3 | Kuweka miongozo ya ushirikishwaji wa taasisi za uwakala wa elimu katika kuratibu fursa za ufadhili wa masomo ndani na nje ya nchi. | Uwepo wa muongozo wa ushirikishwaji.<br><br>Idadi ya fursa za ufadhili zilizoratibiwa. | Juni 2026<br><br>Mei 2026 (endelevu) | Taasisi za Uwakala, Taasisi za Elimu ya Juu na WyEST<br><br>Taasisi za Uwakala |
| 2.5.4 | Taasisi za uwakala wa elimu kubaini fursa za ufadhili zitakazo saidia kuendeleza vipaumbele vya nchi katika kupeleka watanzania kwenda kusoma ndani na nje ya nchi. | Idadi ya mikataba ya makubaliano na taasisi zitakazotoa ufadhili.<br><br>Idadi ya fursa za ufadhili zilizopatikana. | Mei, 2026 (endelevu)<br><br>Machi, 2026 (endelevu) | Taasisi za Uwakala |
| **3** | **USIMAMIZI WA FURSA ZA UFADHILI WA MASOMO NJE YA NCHI** | | | |
| 3.1 | Dawati Maalumu kwa Usimamizi wa Fursa za Ufadhili wa Masomo ndani na Nje ya Nchi. | Uwepo wa dawati na mratibu wa dawati. | Novemba 2025 | WyEST |
| 3.2 | Uhakiki na Uidhinishaji wa Fursa. | Uwepo wa nyezo (tool) ya kufanya uhakiki. | Juni 2026 | WyEST |
| 3.3 | Kupokea Fursa na Kuongeza Uelewa. | Uwepo wa utaratibu wa kupokea fursa na taarifa zake kutoka kwa watoa ufadhili. | Mei 2026 | WyEST |
| 3.4 | Mfumo wa Taarifa na Mrejesho. | Kuwepo kwa ukurasa maalumu wa fursa za ufadhili kwenye tovuti ya WyEST.<br><br>Kuwepo kwa mfumo wa mrejesho wa taarifa. | Desemba 2025 | WyEST |

| | MKAKATI WA KUFANIKISHA MWONGOZO | VIASHIRIA VYA UTEKELEZAJI | KIPINDI CHA UTEKELEZAJI | WAHUSIKA |
|---|---|---|---|---|
| 3.5 | Kuunganisha Mifumo ya Kidijiti. | Uwepo wa Mifumo iliyounganishwa. | Desemba 2025 | WyEST |
| **4** | **KUJENGA UWEZO KWA WAOMBAJI NA WARATIBU WA UFADHILI WA MASOMO** | | | |
| 4.1 | Kujenga uwezo kwa umma. | Kutengeneza utaratibu wa mafunzo juu ya namna na mbinu za uombaji.<br><br>Kuwepo kwa jukwaa la usajili.<br><br>Kufanyika uhamasishaji kwa wazazi. | Juni 2026<br><br>Juni 2026<br><br>Desemba 2025 (endelevu) | WyEST, Taasisi za Uwakala |
| 4.2 | Kujenga uwezo kwa waratibu. | Mafunzo kwa waratibu.<br><br>Mafunzo ya utumiaji mifumo ya kuratibu fursa za ufadhili.<br><br>Mafunzo ya Diplomasia ya Elimu kwa waratibu. | Juni 2026 | WyEST |
| **5** | **KUTANGAZA FURSA ZA UFADHILI WA MASOMO NJE YA NCHI** | | | |
| 5.1 | Kuboresha njia za kutangaza fursa na taarifa zake. | Uwepo wa utaratibu wa kutangaza na kutoa taarifa za fursa. | Desemba 2025 | WyEST |
| 5.2 | Kushiriki na kuandaa makongamano na maonesho. | Kushiriki kwenye makongamano ya elimu na ufadhili. | Juni 2026 | WyEST, Taasisi za Uwakala, Taasisi za Elimu |
| | | Kuandaa kongamano la elimu na ufadhili. | Juni 2026 | WyEST, Taasisi za Uwakala, Taasisi za Elimu |

| | MKAKATI WA KUFANIKISHA MWONGOZO | VIASHIRIA VYA UTEKELEZAJI | KIPINDI CHA UTEKELEZAJI | WAHUSIKA |
|---|---|---|---|---|
| 5.4 | Kutengeneza ukurasa wa fursa kwenye tovuti. | Uwepo wa ukurasa maalumu wa fursa za ufadhili wa masomo kwenye tovuti ya wizara. | Desemba 2025 | WyEST |
| 5.5 | Kushirikiana na jumuiya na washirika. | Uwepo wa mpango kazi wa kushirikiana na wadau kutangaza fursa. | Desemba 2025 | WyEST, Wadau wa elimu |

# Marejeleo

Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu Zanzibar. (2024). *Mpango Mikakati wa Miaka Miwili* 2024/25 - 2025/26. Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu Zanzibar.

CCM. (2025). Ilani ya chama cha mapinduzi ya mwaka 2025/2030.

Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. (2023). Sera ya elimu na mafunzo ya 2014 toleo la 2023.

Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. (2025). Dira ya Taifa ya Maendeleo ya 2050. Dodoma: Tume ya Taifa ya Mipango.

TCU. (2018). *Higher education students admission,enrolment and graduation statistics* 2012/13-2017/18.

TCU. (2019). *Handbook for Standards & Guidelines for University Education in Tanzania (Third Edition).*

TCU. (2021). *Vitalstats on university education in Tanzania*.

TCU. (2023). *Vitalstats on university education in Tanzania*.

UDSM. (2022). Sera ya Umataifishaji ya Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.

UDOM. (2024). Sera ya Umataifishaji ya Chuo Kikuu cha Dodoma.

Umoja wa Afrika. (2024). *Mkakati wa Sayansi, Teknolojia na Ubunifu kwa Afrika.*

Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali. (2024). *Mpango wa Mageuzi ya Sekta ya Elimu, Zanzibar*: Mwaka wa Fedha 2023/24 - 2029/30. Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali, Zanzibar.

**WIZARA YA ELIMU,**
**SAYANSI NA TEKNOLOJIA**

**Mji wa Serikali**
**Mtumba - Mtaa wa Afya**
**S.L.P 10**
**40479 Dodoma, Tanzania**

**info@moe.go.tz**
**www.moe.go.tz**